MWITO PROGRAM

PROG: 1157 KISWAHILI SCRIPT

DURATION:15 MINUTES

MESSAGE:10 MINUTES

SCRIPTURE:ROMANS 8:29

INTRO:

Mpendwa msikilizaji nakualika uwe nami kwa dakika 15 zijazo kwa kipindi hiki ukipendacho cha Mwito.Kipindi hiki ni sehemu ya huduma ya kimataifa yake Mchungaji Harold Williams,kwa jina la Macedonial Call na kimeandaliwa katika studio za Transworld Radio,Nairobi.

Nakukaribisha kwa kipindi cha leo ambacho ni nambari 1157.Ninaamini ulikuwa na wiki njema na sasa uko tayari kwa kipindi hiki.Sina shaka uko na kalamu,bibilia yako pamoja na mahala pa kuandika nasaha kutokana na somo la leo.Naamini umemjulisha rafiki kuhusu kipindi hiki na mnasikiliza pamoja.Kumbuka pia weza kujipatia nakala ya Agano jipya la Bibilia takatifu.Sikiliza hadi mwisho nitakweleza jinsi.

Kwenye kipindi kilichopita tulisoma kutoka aya ***ya 28 ya Warumi sura ya 8….. Nasi twajua kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia meema ,yaani wale walioitwa kwa kusudi lake.***

Ningependa ufungue nami Bibilia yako kwa ajili ya somo la leo .Aya ya 29 ya sura ya 8 ya Kitabu cha Warumi….***Maana wale aliowajua tangu asili aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake,ili yeye naye awe***

mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.Naomba kuongezea aya ya ***30…Na wale aliowachagua tangu asili hao akawaita;na wale aliowaita,hao akawahesabia haki;na wale aliowahesabia haki,hao akawatukuza…***

Naam ni dhahiri kutokana na aya hio kuwa Mungu aliwajua wale ambao aliwachagua tangu asili ili wafananishwe na mwana wake.Nao ndio hao anaowazunumzia kwenye aya ya kwanza ya warumi sura ya 8;kwamba ***wale aliowachagua tangu asili hao akawaita;na wale aliowaita,hao akawahesabia haki;na wale aliowahesabia haki,hao akawatukuza…***

Kwa maneno mengine Mungu anaendelea kumthibitisha kila mwaminio jinsi mfinyanzi wa vyungu afanyavyo na udongo.Na sio kwetu ndugu yangu ,dada yangu kuuliza ni kwa nini Mungu hakutufinyanga hivi au vile.Mbona natapata tabu ,huku wenzangu wakineemeka.Kwa nini nipitie uchungu wa kihisia na mafadhaiko ya kiakili,huku wenzangu wakistarehe? Na mbona nifarakane na jamaa yangu,au watoto wangu,wazazi wangu au ndugu zangu au dada zangu? Wajua nini mwenzangu ,Mungu ametupangia njia katika maisha yetu na tunaweza kuifanya iwe nyepesi au yenye matatizo.Kile anachotamani ni sisi tukubali atufinyange atakavyo,badala ya sisi kuasi,kulia na kunungúnika maishani.Mungu angependa kutufinyanga na kuunda katika umbo la vyombo vya thamani.Jinsi Malaki alivyosema,atakapotufinyanga katika umbo la johari,mwishowe atatengenezea taji kwa mwanawe Kristo itakayorembeshwa na zile johari..johari ambazo ni wana wa Mungu waliosamehewa dhambi zao na kuhesabiwa haki na kufanywa warithi ***kwa neema*** pamoja na Kristo.Yaani mimi na wewe! Wale ambao wameokolewa kwa damu ya Yesu Kristo.Haya yote twashuhudia kupitia maandiko kwenye kitabu ***cha Ufunuo,ambapo Yohana anasema alimwona mwanakondoo aliyekichukua kitabu na wakaimba wimbo usemao..Wastahili mwanakondoo kwa kuwa umetukomboa kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na***

taifa,ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu,nao wanamiliki ṗamoja juu ya nchi

Rafiki yangu Mungu alipanga haya yote na anatupitishia kwenye tanuri ya moto jinsi ya almasi,ambapo anatukata na kutungárisha,na jinsi afanyavyo mfinyanzi anatuuunda katika umbo analolitaka ili hatimaye tupate kufanana naye.Kwa hio hebu nikuhakikishie tena kwamba wewe msikilizaji wangu ulikuwa kwenye mpango wa Mungu tangu mwanzo.Yohana anasema haijafahamika itakavyokuwa ,lakini twajua kuwa atakaporudi Kristo tutafanana naye,kwamba ***….atakuwa mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.*** Yohana anasema aliona umati mkubwa wa waaminio.Alipojaribu kuwahesabu ,hakuweza kumaliza.Hata hivyo itakuwa rahisi sasa kwa Mungu ,ambaye kupitia mwanawe kuwahesabu wana wake.Ni kweli kwamba Mungu anajitayarishia jeshi la wana litakalodhihirishwa siku hiyo.Ni jmbo la kutia moyo tunposikia jinsi maelfu ya watu katika kila pembe ya dunia wanavyotoa maisha yao kwa Kristo.Nina furaha kumtumikia Mungu aliyenijua tangu asili.Mungu yuko katika shughuli nzuri ya kutayarisha watu wake kwa ajili ya siku hiyo.Tunakatwakatwa na kungárshwa ili mswishowe tuweze kuthibitishwa kama johari mbele za Bwana.Chombo kinachostahili kutumika katika nyumba ya Bwana.Naomba nikomee hapo kwa leo ninapokupatia muda wa kulitafakari neno hilo.Lakini sijui kama umeshampokea Kristo kuwa mwokozi wamaisha yako.Ikiwa bado ,fursa ni hii.Tubu dhambi zako na ukajiunge na wenzako ili ujihakikishie uzima wa milele. omba nami ombi hili fupi la toba na nitakuelekeza ya kufanya. … ***Bwana Yesu,naja kwako nilivyo.nimetambua nimekuwa nikiishi maisha ya dhambi.Lakini sasa ninatubu.nisamehe dhambi zangu na unifanye kiumbe kiṗya.ingia ndani ya maisha yangu na kwa roho wako unifinyange na kunifanya kiumbe kiṗya utakavyo.katika jina la yesu nimeomba*** na ***kuamini .Amina***

Sasa naomba ujijujulishe kwa viongozi wako kanisani ikiwa umefanya uamuzi wa kuokoka. Niandikie ili tuweze kufahamiana zaidi. Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na ahata kukupatia vijitabu nan akala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa ukristo wako. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1157.Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari ifwatayo-: 0721 970 520. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 29-30 ya sura ya 8 ya kitabu cha Warumi.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu mtukuka.

Kwaheri.